SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No.16 June 2025

# Mchango wa Mitazamo ya Kiitikadi katika Ujenzi wa Maadili ya Wazanzibari

**Abdi Ramadhan Mberwa**
Mberwaabdi0@gmail.com
*Taasisi Ya Elimu Ya Zanzibar, Wizara Ya Elimu Na Mafunzo Ya Amali, Zanzibar*
*Received Decembre 2024, Accepted: March 2025, published: June 2025*
*© SUMAIT University Journal 2025*

***Abstract*:**

*This paper discusses the contribution of ideological sayings in the building of social values. The aim is to discuss how oral literature through ideological sayings helps to build the values of Zanzibarian. The basic question that guided the research and data analysis is: "What contribution do ideological sayings shape in the Zanzibar community?" Data for this study were collected through interviews and group discussion methods. Furthermore, the data have been analyzed based on a theoretical framework of sociological theory. This paper is presented using qualitative analysis. The findings reveal that ideological sayings are important genres of oral literature that motivate and build love, responsibilities, respect, compassion, and dignity according to the traditions and customs of the Zanzibarian. Therefore, this paper will aim to promote values that uphold respect, solidarity, and integrity.*

**Ikisiri:**

*Makala hii inajadili mchango wa misemo ya kiitikadi katika ujenzi wa maadili ya jamii. Lengo ni kujadili jinsi fasihi simulizi kupitia misemo ya kiitikadi inavyosaidia kujenga maadili ya Wazanzibari. Swali la msingi lililoongoza katika uchunguzi na uchanganuzi wa data linauliza; 'Misemo ya kiitikadi inatoa mchango gani katika ujenzi wa maadili ya jamii ya Wazanzibari?' Swali hilo limeongoza katika ukusanyaji wa data za makala hii ambazo zilipatikana kwa kutumia njia ya usaili na majadiliano ya vikundi. Aidha, data zimechambuliwa kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Sosholojia. Data zimchambuliwa kwa njia ya maelezo. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa misemo ya kiitikadi ni utanzu muhimu wa fasihi simulizi unaohamasisha na kujenga tabia ya uadilifu, upendo, uwajibikaji, heshima, huruma na staha kwa mujibu wa mila na desturi za jamii ya Wazanzibari. Hivyo, utafiti huu utachukua nafasi ya kuendeleza maadili yenye kuzingatia heshima, mshikamano na uadilifu.*

**Keywords:** misemo ya kiitikadi, maadili, uadilifu, jamii ya wazanzibari.

## 1. UTANGULIZI

Waafrika wana utamaduni wao wenye kuonesha hali halisi juu ya maisha yao. [1] anaeleza kuwa sio kweli kwamba utamaduni wa Kiafrika upo bila ya mwelekeo wowote, bali upo katika hali ya kukua na kuendelea kutokana na mwingiliano na uhusiano wa watu. Moja kati ya vielelezo vinavyoonesha mila na amali za jamii ni fasihi. Misemo ya kiitikadi ni sanaa muhimu ya fasihi katika utamaduni wa watu. Mara nyingi misemo ya kiitikadi hutumika kuonesha mitazamo ya jamii

kuhusu mambo ya kijamii, kisiasa, na kiutamaduni. Katika jamii nyingi, hasa za Kiafrika, misemo ya kiitikadi hutumika kutoa miongozo ya kimaisha.

Wazanzibari ni watu wenye utajiri wa historia na utamaduni. Katika mazingira ya Zanzibar, misemo ya kiitikadi ni njia maarufu ya kufikisha ujumbe na urithi wa jamii. Baadhi ya wakati misemo ya kiitikadi hutumika kufundisha, kulea na kuimarisha tabia njema. Ijapokuwa wataalamu kama vile [2] na [3] ameandika kuhusu misemo ya kiitikadi, lakini hakubainika aliyeihusisha na ujenzi wa maadili. Hivyo basi, makala hii imechunguza mchango wa misemo ya kiitikadi katika ujenzi wa maadili ya Wazanzibari.

### *1.1 Methodolojia na Nadharia*

Data za makala hii zimechambuliwa kwa kutumia Nadharia ya Sosholojia iliyoasisiwa na mwanafalsafa wa Kifaransa mnamo karne ya kumi na tisa anayeitwa Auguste Come. Msingi Nadharia hii imesaidia kufafanua jinsi misemo ya kiitikadi inavyochangia ujenzi wa maadili ya jamii ya Wazanzibari. Aidha, mbinu ya usaili pamoja na majadiliano ya vikundi zilitumika katika kukusanyia data za utafiti huu.

### *1.2 Dhana ya Misemo ya Kiitikadi*

Misemo ya kiitikadi ni miongoni mwa vipera vya misemo vinavyoujenga utanzu wa semi. Kazi yake kuu ni kuelimisha, kuadilisha, kuonya, kuburudisha na kurithisha utamaduni. Misemo ya kiitikadi imeelezwa na kufafanuliwa na wataalamu mbalimbali. [4] anaeleza kuwa misemo ya kiitikadi ni imani za wenyeji na mambo mengine wanayoyasadiki kama imani za ushirikina ambapo kwa asili yanatokana na maarifa au hata vitendo vya kawaida. [5] na [6] wanaeleza kwamba ni kauli za kiitikadi zinazotoa muongozo wa kiimani katika kujenga inayokubalika na wanajamii ili kuepukana na balaa na madhara mbalimbali.

Kwa hivyo, misemo ya kiitikadi ni misemo inayoeleza imani ya watu kuhusu jambo fulani. Kwa kawaida misemo hii husawiriwa kwa kuangalia miktadha mbalimbali ya kimaisha. Makala hii imekusanya jumla ya misemo ya kiitikadi kumi na nne ambayo imehusika katika uchambuzi na uchanganuzi wa data. Misemo yenyewe ni ifuatayo:

1. Ukimcheka mkweo utaota chokea.
2. Mama mzazi akitoka kabla ya siku saba baada ya kujifungua atapatwa na madhara mzazi au mwana mchanga.
3. Biharusi akiazia na msiba baada ya ndoa ni nuksi na mkosi katika ndoa.
4. Kumwita mtu kwa jina lake ndani ya pango la Miza wa Miza na akiitikia atageuka jiwe [1].
5. Mtoto mchanga akiachwa peke yake atageuzwa na shetani.
6. Kuzoea kulala na kufutika mikono mapajani utakuwa masikini.
7. Mtu akilala pasipo na kuosha miguu, nyayo zake zitarambwa na shetani.
8. Kila penye kundi lazima awepo kiongozi na pasipokuwa na kiongozi huongozwa na shetani
9. Kumtukana Sharifu kunapopotosha[2] midomo

---

[1] Ni pango lililoko Kizimkazi Dimbani lenye simulizi za kale za mtu na mke mweza walipochota maji katika pango ambalo lina miiko. Mwiko mmojawapo ni haikuruhusiwa kuitikia ukiwa pangoni. Kutokana na sababu za wivu, mke mdogo alimuita mke mweziwe kwa sauti. Mara baada ya mke mkubwa kuitikia aligeuka jiwe. Hivyo, mke mdogo akapata fursa ya kuishi na mume peke yake.

10. Mzee akiteleza na kuanguka ni dalili kuwa atakufa mtu
11. Mwanamke mwenye mimba akiangalia au kufuata jeneza la maiti atakatisha maisha ya mtoto wake wa tumboni.
12. Mwenye kumcheka mkwewe hupata maradhi ya chokea
13. Mwanamke akiwa ndani ya siku zake havuki maji (bahari) Mkokotoni kwenda Tumbatu au Tumbatu kwenda Mkokotoni, akivuka chombo kitazama baharini
14. Kuchungulia mtu mzima aliyekaa vibaya (uchi) kunaleta upofu.

### *1.3 Maadili*

Maadili ni maoni ya wanajamii juu ya mambo na matendo yanayokubalika na wengi na kuonekana kuwa na maslahi ya kujenga heshima haki na usawa kwa mujibu wa utamaduni wao [7]. Aidha, [8] na [9] wanaeleza kuwa maadili ni dhana ya kufikirika inayotumika kama kanuni za jumla zinazoongoza katika kutenda matendo pamoja na tabia. Maana hii inaonesha kuwa maadili ni jambo linalofungamana na maslahi ya kihisia katika kuimarisha mustakabali wa maisha ya jamii. Naye, [10] wanasema kuwa maadili ni mfumo wa thamani ya jamii ambao hutumika kama hatua ya kumbukumbu na mwongozo katika shughuli za kimaisha. Kutokana na maana hizo za wataalamu hao, tunaweza kufasili maadili kama kanuni au viwango vya tabia nzuri na sahihi vinavyomuongoza mtu au jamii katika mwenendo na tabia.

## 2.0 JINSI MISEMO YA KIITIKADI INAVYOJENGA MAADILI YA JAMII

Kwa kawaida misemo ya kiitikadi hutumiwa na jamii ya Wazanzibari kama njia muhimu ya kufikisha maarifa na mafundisho ya kimaadili kutoka kizazi hadi kizazi. Kwa hivyo, misemo hii husaidia kujenga maadili ya jamii ya Wazanzibari kupitia vipengele vifuatayo:

### 2.1 Uadilifu

Uadilifu ni hali ya mtu kufanya haki bila ya kuegemea upande mmoja [11]. Uadilifu ni msingi wa ujenzi wa maadili. Mathalani, ujenzi wa jamii bora, malezi na uongozi bora unategemea uadilifu wa watu katika matendo yao. Udhaifu wa uadilifu ni mporomoko wa maadili ya jamii [12]. Kutokana na umuhimu wa uadilifu, wazee hutamani watoto wao kuongoka katika uadilifu ili kuwa na jamii imara. Kwa mfano wazee wanasema: "*Ukimcheka mkweo utaota chokea*"

Msemo huu una maana kuwa mtu mwenya kucheka mkwe wake awe wa kiume au wa kike atapata maradhi ya chokea[3]. Msemo huu unasisitiza kutoa heshima kwa pande zote mbili za wazazi na kutoonesha dharau. Huu ni mtazamo katika kuchunga maadili ya kijamii katika familia. Endapo moja wa wanandoa kukosa uadilifu mbele ya wazazi wa mwenzake ni chanzo ukosefu wa upendo kwa wanandoa pamoja na wazazi wa wanadoa. Kwa mantiki hiyo kuchunga na kufuata uadilifu kama huu kwa kuzingatia mtazamo wa imani ya malezi utachangia kujenga maadili ya jamii na kuwa na familia yenye umoja na mshikamano. Msemo mwengine wa uadilifu ambao unaweza kujenga maadili ya jamii ni ule usemao: "Mama mzazi akitoka kabla ya siku saba baada ya kujifungua atapatwa na madhara mzazi au mwana mchanga".

[2] Ulemavu wa midomo; kupata madhara mdomo wa juu au wa chini kwa kuvimba au kupata ulemavu wa kukaa upande.
[3] Ni upole unaofanyika katika ugozi wa ujuu au wa chini ya jicho ambao humfanya mtu kuvimba jicho.

Huu ni msemo wa kiitikadi ambao baadhi ya jamii ya Wazanzibari wanauamini na kuutekeleza kwa vitendo. Isitoshe, hii ni mila na desturi ya asili ya Wazanzibari kukaa ndani siku saba kwa mama mzazi baada ya kujifungua. Mila hii imejengwa na imani kwamba kama mtu akienda kinyume na kanuni hiyo mzazi au mtoto atadhurika. Msemo huu unaonesha uadilifu katika matunzo ya mama mzazi na mwanawe. Kinyume chake, yaani kutoka nje na kufanya kazi nzito ni kudhoofisha afya na siha ya mama na mtoto. Kwa upande mwengine, wazee wa mzazi wanawajibika kuwa na upendo na huruma kwa mzazi aliyejifungua ili asijedhurika. Hivyo ukosefu wa uadilifu wa huduma nzuri ya jamaa wa mzazi ni chanzo cha uporomoshaji wa maadili ya jamii hususani katika malezi.

Kwa ufupi msemo wa kuanza kula bila kusema bismillah na msemo unaomkataza mzazi kutoka nje siku saba baada ya kuzaa unawaelekeza watu katika kujenga tabia ya uadilifu ndani ya nyoyo za wanajamii. Kwa mujibu wa [13] wanaeleza kuwa mfumo wa fikra unaozingatia uadilifu ni msingi wa tabia njema. Hali hii itasaidia kujenga mitazamo yenye kuheshimu mila na desturi za jamii. Kwa maana hiyo, wazee kutumia misemo ya kiitikadi ikiwa kama mbinu ya kuendeleza uadilifu na kujenga tabia njema katika jamii. Hivyo, suala la uadilifu katika ujenzi wa maadili ni nguzo ya msingi na yenye thamani inayohitajika kuendelezwa na kufanyiwa tafakari kama ilivyotiliwa mkazo na nadharia ya sosholojia kuwa jamii inahitaji maadili ya uadilifu ili kuwepo na utulivu na usawa.

## 2.2 Upendo

Suala la upendo katika ujenzi wa maendeleo ya jamii ni kitu kisichopingika. Ili jamii iendelee hapana budi kuwepo kwa upendo baina ya familia, jamii na taifa. [14] anaeleza kuwa Keneth Kaunda aliwapongeza Waafrika kutokana na mafanikio yao ya kung'oa na kuushinda ukoloni kwa sababu ya utu na upendo wa bara lao na wala sio nguvu za jeshi imara na silaha kali. Kwa maana hiyo, upendo ni msingi wa kutunza, kuendeleza na kudumisha kitu, mtu au jambo. Kwa vile jamii ya Wazanzibari ni watu wenye mila na desturi zinazohikimiza upendo baina yao. Wazee hawakusahau kutumia misemo kadhaa ya kiitikadi katika kutilia mkazo suala la upendo katika jamii ili kujenga maadili yao. Mathalani, pale waliposema: *"Biharusi akianzia na msiba baada ya ndoa ni nuksi na mkosi katika ndoa*".

Wazee hutumia msemo huu ili kuonesha njia ya mafanikio ya kimaisha. Wanatumia msemo kwa kuwajenga wanajamii kiimani. Wazee waliamini kwamba pasi na kumjenga mtu kiimani ni vigumu kumwongoza. Hivyo, msemo umetumika kiishara ikiwa kama kanuni au sheria ya kupunguza utokeaji wa migogoro na matatizo mwanzoni mwa ndoa au jambo jengine lolote lile. Ijapokuwa msemo umetumia 'biharusi' lakini neno hilo linaweza kutumika hata katika mazingira mengine kama ishara ya jambo jipya wakati harusi ni furaha na msiba ni huzuni. Ni dhahiri kwamba hakuna hata mtu mmoja anayependa kukumbana na matatizo, shida na maafa mwanzoni mwa jambo lake, kwani hali hiyo inaweza kukatisha tamaa pamoja na kupunguza ari na imani ya utendaji wa jambo.

Hata katika maisha ya ndoa kama ilivyojitokeza katika msemo wa hapo juu, imeonekana kuwa na lengo la kuimarisha mapenzi na kupunguza idadi ya talaka katika jamii. Katika mazingira ya maisha ya ndoa, biharusi hana budi kuficha aibu zake kwa mume, kadhalika na bwana harusi kwa mke ili kuimarisha mapenzi, kinyume na hivyo maisha ya ndoa huwa na wakati mgumu. Kwa hivyo, msemo umekuwa kama angalizo la maisha ili kuchunga maadili ya jamii.Mmsemo mwengine unasaidia kujenga maadili ya jamii ni ule usemao: "*Kumwita mtu kwa jina lake ndani ya pango la Miza wa Miza mtu huyo atageuka jiwe".*

Msemo huu wa kiitikadi unaonesha jinsi jamii inavyojali siha, afya na usalama wa mtu. Hali hiyo inatokana na imani ya upendo inayojitokeza katika msemo huu. Kwa kawaida, utamaduni wa Wazanzibari unawaiminisha kwamba, pango mara nyingi hutumika kwa shughuli za kimila. Pamoja na hilo, ni moja kati sehemu inayohitaji utulifu na ukimya wa hali ya juu. Hata kama, wazee wanakataza kuitana majina kwa sauti kutokana na imani ya mtu atageuka jiwe lakini ni fantasia ili kuepusha zogo, kwani mazingira ya pango ni ya viumbe wengi wa hatari kwa maisha ya binadamu. Msemo mwengine unaweza kujenga maadili kwa kupitia upendo wa wanajamii ni ule unaosema: "*Mtoto mchanga akiachwa peke yake atageuzwa na shetani*".

Msemo huu wa kiitikadi unaonesha upendo katika jamii, hususani kwa watoto wachanga. Msemo huu unafundisha kulea na kutunza mtoto mchanga au mdogo ili aepukane na madhara na majanga mbalimbali yatakayohatarisha uhai au maisha yake. Katika muktadha huu, mtoto mchanga ni mfano wa kiumbe: yaani binadamu aliye na uwezo mdogo wa kuelewa hatari na kujua njia sahihi kulinganisha na kijana au mtu mzima. Hivyo, msemo unatoa wito kwa wazazi, walezi, au jamii kwa ujumla kuwa karibu na watoto. Kuwajali ni dalili ya upendo ambao utasababisha kupata vijana wema walioongoka kimaadili. Kinyume chake, yaani mtoto akiachwa peke yake atageuzwa na shetani kutokana na kupokea mambo mbalimbali. Hatimaye, kupotoshwa na nguvu hasi na kuchukua tabia mbaya na matendo maovu.

Hivyo basi, utafiti umebaini kuwa suala la upendo linafaa kuanzia ngazi ya familia. Kwa mfano, kitendo cha utelekezaji wa watoto wachanga. Hii ni dalili ya ukosefu wa upendo kwa wazazi. Ikiwa upendo kama dhana ya kijamii na muhimu kwa kuunda uhusiano mzuri kati ya watu, jamii ya Wazanzibari inachukuliwa kama msingi wa uhusiano wa familia na jamii kwa ujumla. Kwa hivyo, misemo hii mitatu inaonesha upendo ambapo ni msingi wa ujenzi wa maadili ya jamii, kwani ukosefu wa upendo ni chanzo chuki na migogoro ambapo ni dalili uvunjifu wa maadili ya jamii ya Wazanzibari.

### 2.3 Uwajibikaji

Uwajibikaji ni hali ya mtu au kikundi cha watu kuelewa na kutekeleza majukumu yao kwa bidii, uwazi, uadilifu na uthibitisho wa matokeo. Aidha, uwajibikaji ni kuheshimu majukumu ya mtu kwa ngazi ya familia, jamii au taifa. Katika suala la uwajibikaji, wazee wanawaelekeza wanajamii kujituma kwa mujibu wa mila na desturi za jamii. Kwa hivyo, uwajibikaji ni jambo muhimu linalochangia ufanisi na ustawi katika maeneo mengi ya maisha, iwe ngazi ya familia, jamii au serikali. Kutokana na umuhimu huo wazee wanasema: "*Kuzoea kulala na kufutika mikono mapajani utakuwa masikini".*

Huu ni msemo wa Kiswahili wa kiitikadi unaoelekeza utaratibu wa kulala kwa jamii ya Wazanzibari. Kulala ni kitendo cha kawaida katika maisha ya binadamu, pia ni sehemu ya mapumziko ya viungo baada ya kufanyakazi. Jamii inakatazwa kulala na kufundika mikono mapajani kwa imani ya kwamba itakuwa unakaribisha umasikini. Wazee wanautumia msemo huu kiishara kwa kuhusisha na uvivu. [15] anaeleza kuwa mtu akilala na mikono kuiweka mapajani ataona uvivu kuondoka mapema kwa ajili ya kwenda kufanyakazi yake ya kumpatia riziki. Kwa hivyo, ili kujenga maadili katika jamii hakuna budi suala la uwajibikaji liwe katika mstari wa mbele. Kutokuwepo kwa uwajibikaji kunaweza kuibua wizi, uzururaji na ubakaji katika jamii.

Msemo mwengine unaoeleza kuhusu uwajibikaji ni ule unaosema: "*Mtu akilala pasipo na kuosha miguu, nyayo zake zitarambwa na shetani*". Msemo huu unadokeza suala la usafi wa mwili, kwani kuosha miguu wakati wa kulala ni sehemu ya usafi na kinyume chake ni uchafu. Katika malezi, wazazi wana jukumu la kufundisha watoto wao usafi ili kupata kizazi chenye tabia njema na afya bora. Kwa vile, usafi ni kitu muhimu kwa afya ya binadamu, wazee waliona haja ya kutumia msemo wa kiimani kama huu ili kuondosha tatizo la watoto na vijana kulala bila kuosha miguu. Katika ujenzi wa jamii mpya, suala la usafi halifikiwi kirahisi, hivyo panahitajika utayari wa watu wa kulishughulikia. Vilevile, kulala bila kuosha miguu ni ishara ya uvivu. Kwa hivyo, uvivu ni jambo la kupigwa vita katika jamii kwa sababu unaweza kuathiri maendeleo ya mtoto au jamii kwa ujumla.

Kwa mantiki hiyo, uwajibikaji ni nguzo muhimu katika maendeleo ya kifamilia, kijamii na kitaifa. Bila ya uwajibikaji katika jamii kunaweza kujenga jamii iliyokosa maadili na hatimaye, kuathirika kwa jamii. Hivyo, uwajibikaji sio tu jukumu la mtu binafsi, bali ni suala linalogusa ustawi wa jamii nzima ambalo linahitaji ushirikiano wa pamoja ili kuleta mafanikio na maendeleo endelevu ya mtu binafsi pamoja na jamii nzima.

## 2.4 Heshima

Heshima ni kitendo cha kuthamini na kujali utu wa mtu bila kujali tofauti za kiumri, elimu, kabila na cheo. Isitoshe, heshima inahusisha hali ya kuwa na nidhamu kwa wengine na kuthamini tofauti zao za kiutamaduni, kijamii na kifalsafa. Wazee hutumia misemo ya kiitikadi ambayo inasaidia kuhimiza watu wao kujenga heshima kwa wakubwa na viongozi, kuwa mtiifu kwa kufanya yanayokubalika na kuacha yasiyokubalika katika jamii. Pia, kupitia misemo ya kiitikadi jamii inaelezwa kuheshimu wazazi na kuonywa kutowakemea, kutowakera na kutowadhalilisha. Kwa mfano, misemo ifuatayo inadhihirisha michango yao katika ujenzi wa maadili kupitia heshima kama vile: "Kila penye kundi lazima awepo kiongozi na pasipokuwa na kiongozi huongozwa na shetani".

Msemo huu, unatoa wito kwa jamii kuhusu umuhimu wa uongozi katika jamii kwa kusisitiza kuwa bila uongozi, watu wanaweza kufuata mwelekeo uliyokuwa sio sahihi. Katika muktadha wa ujenzi wa maadili, msemo huu unaonesha nafasi ya heshima kwa kiongozi. Hii inamaana kwamba ikiwa kila mtu kiongozi, katika sehemu itakosekana heshima: yaani kila mmoja anajiona mkubwa. Msemo huu wa kiitikadi unaonesha jinsi jamii inavyotakiwa kuwa na heshima ambayo itasababisha kupata kiongozi anayekubalika. Hali hiyo itachangia ujenzi wa maadili kutokana na kuwa kiongozi katika jamii ni kigezo chema na mfano wa kuigwa. Hivyo, anapaswa kuwa na tabia njema zitakazoshawishi wafuasi wake kuiga na kuwa kielelezo cha jamii. Bila ya kuwa na kiongozi mwenye heshima, watu wanaweza kupotea njia.

Kwa hivyo, msemo huu unaonesha kwamba ili jamii au kundi liendelee kimaadili, ni muhimu kuwepo kwa heshima ambayo itasaidia kupata viongozi wenye tabia njema. Pia, msemo huu unaweza kusaidia kujenga maadili kupitia heshima kutokana na kuhusishwa na dhana ya utawala bora na viongozi wenye uwezo wa kuongoza kwa haki na kwa manufaa ya wote. Maadili ya uongozi hujengwa kwa heshima ambayo inatokana na nidhamu na uaminifu wake juu ya jambo linalochochea mafanikio ya pamoja katika jamii. Tatu, heshima huzalisha kiongozi mwenye maadili kutokana na ushawishi wake mzuri kwa watu wa jamii iliyomzunguka. Kwa maana hiyo, msemo huu unasisitiza kwamba heshima ni muhimu katika mchakato wa kujenga na kuendeleza maadili ya

jamii. Ieleweke kwamba pasipo na heshima hapatokuwa na kiongozi mzuri, hali itakayopelekea jamii kuongozwa na nguvu za giza, mfano wa shetani.

Vilevile, wazee wanasema: "Kumtukana Sharifu kunapopotosha midomo". Mawazo ya watoataarifa kuhusu msemo huu wa kiitikadi yamewafikiana kwamba sharifu ni ishara ya kiongozi au mkuu yoyote katika ngazi ya familia, ukoo, jamii au taifa. Msemo ulielezewa kuwa ni wa kifantasia ambapo wazee mara nyingi hutumia katika muktadha wa kuonesha heshima kwa utawala, wakubwa na viongozi ili kuenzi mamlaka husika. Kwa ujumla msemo huu unachangia ujenzi wa maadili ya jamii kutokana na kukazia suala la heshima kwa kutumia balagha ya mtu kupata ulemavu wa mdomo endapo ataondosha heshima kwa mkubwa wake. Hata hivyo, huu ni msemo unaotumika kuchunga na kuendeleza mila na desturi ya jamii ya Wazanzibari ya heshima kwa wakubwa. Sambamba na msemo huu, wazee pia wanasema: "*Mzee akiteleza na kuanguka ni dalili kuwa atakufa mtu".*

Kwa mujibu wa data zilizokusanywa kupitia msemo huu zimeonesha heshima katika muktadha wa malezi ili kujenga nidhamu kwa wazee. Aidha, watoataarifa wameeleza kuwa katika mazingira ya kawaida hakuna uhusiano kati ya kuanguka kwa mzee na tukio la kifo cha mtu mtaani. Huu ni ubunifu wa sanaa ya kifasihi unaotumiwa na wazee katika kuleta nidhamu na heshima kwa wakubwa. Hivyo, kusema kuanguka kwa mzee ni dalili ya kufa mtu ni kuitia hofu na taharuki jamii ili kuepusha kejeli na dharau kwa wazee pindi wanapopata shida au matatizo. Kwa maana hiyo, imani na matumizi ya msemo huu katika jamii ni kujenga maadili.

Kwa ujumla, heshima ni nguzo muhimu katika ujenzi wa maadili na utawala bora. Heshima haijumuishi tu kuthamini utu wa mtu, bali pia inahusisha kujali na kuzingatia tofauti za kiutamaduni, kijamii na kifalsafa. Kadhalika, heshima ni nguzo ya msingi katika ujenzi wa misingi ya uongozi wa kimaadili. Kiongozi anatakiwa kuwa mfano bora kwa jamii. Heshima ni muhimu kwa maendeleo ya kijamii, kwani bila ya heshima, jamii haitoweza kupata maendeleo. Hivyo, kupitia heshima, jamii itaweza kupata viongozi wa kweli, wenye tamaa za maendeleo ya jamii na uwezo wa kuongoza kwa haki na kwa manufaa ya wote.

### 2.5 Huruma

Huruma ni hali ya kuwa na moyo wa kuelewa na kutoa msaada kwa yule anayehitaji msaada. Huruma ni jambo muhimu katika kujenga maadili ya jamii kwani ndiyo inayoweza kusaidia uboreshaji na uimarishaji wa uhusiano wa kijamii na kujenga mshikamano. Aidha, huruma ni uwezo wa kuelewa na kujali hisia na hali za watu au viumbe wengine. Vilevile, huruma ni sehemu muhimu ya maadili kama vile usawa, haki, na mshikamano. Katika jamii, huruma inatoa mchango mkubwa katika kupunguza migogoro, kukuza uhusiano wa kiraia, na kuboresha hali ya ustawi wa kila mtu. Hivyo basi, kupitia misemo ya kiitikadi huruma inaoneshwa kama ifuatavyo: "*Mwanamke mwenye mimba akiangalia au kufuata jeneza la maiti atakatisha maisha ya mtoto wake wa tumboni".*

Kwa mujibu wa data za msemo huu zimeonesha ujitokezaji wa huruma katika muktadha wa hofu juu ya majanga na balaa kutokana na mtazamo wa imani ya jamii juu ya uwezo na nguvu za maiti. Ama wale wa hofu ya majanga na balaa ni kwa sababu ya udhaifu wa mwanamke katika subira. Hivyo, kuliona jeneza alilotiwa maiti anaweza kupata mshituko wa moyo ambao utasababisha athari kwa mzazi na mtoto aliye tumboni. Aidha, kwa wale wa imani juu ya uwezo wa maiti

walisema kuwa maiti ana uwezo wa kusikia na kujua matendo yanayofanywa na viumbe hai. Hivyo kuna uwezekano wa kuwasiliana kati ya maiti na mtoto aliye tumboni.

Pamoja na hayo utafiti umebaini kuwa msemo huu unaonesha huruma ya kuwajali wajawazito kutokana na hali ngumu ya kipindi hicho. Wazee wanaelewa kuwa kipindi cha ujauzito kinahitaji utulivu wa kimwili na kiakili pamoja na afya njema. Hivyo, kushiriki, kuona au kusikia matukio yanayoweza kujenga hofu, woga, simanzi na taharuki ni hatari kwa afya ya mama mjamzito. Hivyo, msemo huu unaonesha huruma ambayo inasaidia kujenga maadili katika jamii.

### 2.6 Staha

Staha ni msingi wa maadili ya jamii yenye umoja na amani. Kama jamii itajitahidi kuweka staha mbele katika maadili yake, basi itakuwa na nguvu ya kushinda changamoto yoyote inayoweza kutokea. Staha ni hali ya kujiepusha na tabia za aibu au zinazoweza kudhalilisha utu wa mtu. Staha katika jamii haizungumzwi katika mazungumzo ya kawaida pekee bali hata kupitia fasihi. Kwa mfano, misemo ya kiitikadi ni miongoni mwa kazi za fasihi simulizi zinazojikita katika kuonesha staha juu ya utu wa mtu. Mathalani, wazee wanasema: "*Mwenye kumcheka mkwewe hupata maradhi ya chokea"*

Msemo huu unaonesha umuhimu wa staha katika jamii, hususani katika mahusiano ya familia. Msemo huu una maana kwamba mtu anayecheka, kudhihaki, au kutukana mwingine, hasa katika familia, atapata madhara au matatizo katika maisha yake. Hii inaonesha tabia ya kutokuwa na staha haifai kwa maendeleo ya jamii. Aidha, staha ni kama nguzo ya ujenzi wa maadili ya jamii bora. Katika jamii yoyote ile, watu wanategemea ulinzi, heshima na haki. Kwa maana hiyo, mtu anapokuwa na tabia ya kudhihaki au kumdharau mwingine, hasa katika familia, ni ukosefu wa staha na uvunjifu wa maadili ya jamii.

Kwa kifupi, msemo huu wa kiitikadi unasisitiza kuwa staha ni tabia njema katika ujenzi wa maadili ya jamii. Watu wanapaswa kujiepusha na dhihaki, kicheko, au matusi kwa wengine, kwani athari za tabia hizo ni kushusha maadili ya jamii na hatimaye kujenga chuki, dharau na migogoro. "*Mwanamke akiwa ndani ya siku zake havuki maji (bahari) Mkokotoni kwenda Tumbatu au Tumbatu kwenda Mkokotoni, akivuka chombo kitazama baharini".*

Msemo huu, una maana pana na unagusia masuala ya staha katika ujenzi wa maadili ya jamii. Hali hiyo inajitokeza hasa linapokuja suala la nafasi ya mwanamke katika jamii na jinsi anavyohusishwa na mazingira yake. Msemo huu unahusishwa na imani za kitamaduni na mila za jamii kuhusu wanawake, ingawa baadhi ya vipengele vya msemo huu vinaweza kuwa na tafsiri za kijamii au kidini. Msemo huu umetumika kama ishara ya staha na heshima kwa mwanamke kwa kuzingatia muktadha wa tabia zake katika jamii. Mwanamke akiwa ndani ya siku zake[4] kuna mambo ambayo jamii inadhani ni ya muhimu kwake kuepuka ili kuhifadhi heshima yake na ya familia yake. Kwa mfano, baadhi ya tamaduni, mwanamke anayeenda kinyume na kanuni hizi za kijamii au kidini anakuwa anaonesha ukosefu wa staha kwa watu wa karibu na jamii kwa ujumla.

[4] Hedhi (ada ya mwezi) au nifasi (ada ya baada ya kuzaa)

Pamoja na hayo, mantiki iliyokusudiwa katika msemo huu kuhusisha na kuvuka kwenda Tumbatu[5] ni sababu ya kuepusha aibu kwa mwanamke. Pia, tamaduni nyengine zinawakataza wanawake kuepuka safari kubwa au kazi kubwa wakati wa hedhi ili kuzuia matatizo yanayoweza kutokea na kuonekana kama udhaifu au ukosefu wa staha. Ijapokuwa baadhi ya imani hizi zinaweza kuonekana kama vikwazo lakini ni muhimu kutafakari nafasi yake katika kuleta staha na usawa katika jamii ili kujenga maadili ya jamii.

Pia wazee wanasema: "*Kuchungulia mtu mzima aliyekaa vibaya (uchi) kunaleta upofu*". Msemo huu, unazungumzia madhara ya kuingilia faragha ya mtu mwengine. Kitendo cha kuingilia faragha ya mtu ni kuonesha uvunjifu wa staha ya mtu ambapo ni kinyume cha maadili ya jamii. Msemo huu wa kiitikadi unasisitiza umuhimu wa kuwa na staha katika kujenga maadili ya jamii. Katika jamii, staha ni msingi wa kudumisha amani, heshima, na umoja. Kuchungulia ili kujua udhaifu, makosa au siri ya mtu mwengine ni kuingilia faragha ya mtu na ni kuondosha staha na inaweza kuwa chanzo cha migogoro katika jamii. Jamii yenye maadili na ustawi, ni muhimu kuwa na heshima kwa faragha na utu wa kila mtu. Kwa hivyo, kuchungulia kwa njia yoyote ile, sio tu kunaleta madhara kwa mtu anayechunguliwa, bali pia kuvunja staha. Kwa maana hiyo, jamii inapaswa kuimarisha staha ili kuepukana na tabia zinazoweza kuvuruga amani na ushirikiano wa kijamii.

## 3.0 HITIMISHO

Mjadala huu unathibitisha kuwa misemo ya kiitikadi si tu ni misemo ya kisanaa, bali ni nyenzo muhimu za kuhamasisha na kufundisha maadili katika jamii. Kwa kuzingatia mantiki ya misemo na kufuata misemo hii, jamii inaweza kufanikiwa kujenga na kudumisha maadili kupitia uadilifu, yaani Utafiti umebaini kuwa Wazanzibari wanatakiwa kuondosha dharau kwa wazazi wa mke au wa mume. Aidha, umebaini kuwa ni fantasia. Hata hivyo, msemo umekuwa kama chombo cha kuwekea nidhamu na utulivu. upendo, uadilifu, heshima, huruma, uwajibikaji, na staha, ambayo ni mambo muhimu kwa ustawi wa familia, jamii, na taifa kwa ujumla. Aidha, kipengele cha misemo ya kiitikadi kinahitaji kufanyiwa tafiti zaidi, kwani ni kipengele kinachoanza kusahaulika kama anavyoeleza Farsi kuwa kutokana ujio wa elimu ya kisasa mafunzo yatokanayo na itikadi yanapotea.

[5] Kisiwa kilichopo kaskazini mwa kisiwa cha Unguja, Zanziba Tanzania, katika Bahari ya Hindi. Kisiwa hiki ni sehemu ya Mkoa wa Kaskazini Unguja, na kinapatikana kando ya pwani ya Unguja, ambapo ni kisiwa kikuu cha Zanzibar.

**MAREJELEO**


[1] W. J. Ndaba. (1994). Ubuntu in comparison to western philosophies. Ubuntu School

[2] L. Harries. (1965). Swahili prose texts. Exford University Press.

[3] T. S. Y. Sengo. (1995). Itikadi katika jamii za Kiswahili: Lugha, utamaduni na fasihi ya Kiswahili. TUKI.

[4] S. S. Farsi. (1958). Swahili Sayings from Zanzibar (2): Riddles and Superstitions. Nairobi: East Africa Publication.

[5] C. Fershtman, U. Gneezy & M. Hoffman. (2011). Taboos and identity: considering the unthinkable. Microeconomic. 3, 139 – 164.

[6] M. D. Shongwe. (2015). “Kulinganisha Miiko na Tasfida ya Waswahili (Wajomvu) na Warabai”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi.

[7] T. Bennett. (2015). Cultural Studies and the Culture Concept. Cultural Studies. 29(4), 546 – 568.

[8] W. S. Logan. (2016). Cultural Diversity, Heritage and Human Rights. International Heritage Studies, 18(3) 1 – 14.

[9] J. Gibson. (2017). Creating Selves: Intellectual Property and the Narration of Culture. New York: Routledge.

[10] Q. H. Vuong na wenzake (2018. Cultural additivity: behavioural insights from the interaction of confucianism, buddhism and taoism in folktales. Palgrave Communication, 4(1), 1 – 15.

[11] BAKIZA. (2010). *Kamusi la Kiswahili fasaha*. Oxford University Press.

[12] I. Kant. (1997). Groundwork of the Metaphysics of Morals (M. Gregor, Translator). London: Cambridge University Press.

[13] T. S. Y. Sengo & S. S. M. Bathawab. (2007). Utendi wa Mambo Mambo. Dar es Salaam: Al-Amin Education and Research Academy

[14] F. E. Ekanem. (2012). On the ontology of philosophy. Medwell, 9(6), 306 – 310.

[15] D. O. Ajakaiye & V. A. Adeyeye. (2002). Concepts, measurements and causes of poverty. *CBN Economic & Review*. 39(4), 1 – 32.